

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1
Nukushi: 255-262961502
Baruapepe : press@ikulu.go.tz
Tovuti : www.ikulu.go.tz



OFISI YA RAIS,
IKULU,
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,
CHAMWINO,
S.L.P 1102,
40400 DODOMA.

Morogoro
05 Agosti, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitaka Wizara ya Kilimo kuptitia Wakala wa Uhifadhi wa Chakula (NFRA) kununua mpunga kwa bei ya Shilingi 900 kutoka 570 ambayo itakuwa na tija kwa Mkulima kama ambavyo ilikuwa ombi kwa Rais toka kwa Wakulima wa bonde la Kilombero.

Rais Dkt. Samia amesema hayo leo wakati akizungumza na wananchi wa Ifakara katika mkuutano wa hadhara uliofanyika katika Uwanja wa CCM Ifakara Mji, Wilaya ya Kilombero.

Rais Dkt. Samia pia amesema Serikali itaendelea kuwapelekea wakulima wa Kilombero pembejeo za kilimo na kukamilisha miradi ya umwagiliaji inayotekelizwa ili kuwaongezea tija katika kilimo.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema Serikali inafanya kazi miradi mbalimbali Wilayani hapo ikiwemo kukarabati skimu ya Idete pamoja na kuchimba na kujenga miundombinu ya maji ya Kilombero Block Farm.

Hali kadhalika, Rais Dkt. Samia amewahimiza wananchi hao kuzalisha kwa wingi kwa kuwa soko lipo na Serikali inatoa ruzuku.

Aidha, Rais Dkt. Samia amewataka wananchi kujivekeea akiba wanapopata fedha za mavuno na pia kujikatia bima ya afya ili wao na familia zao wanufaike na huduma za afya zilizoboreshwa mwaka mzima.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read "Sharifa B. Nyanga".

Sharifa B. Nyanga
Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

